Afisi Kuu ya Habari

بسم الله الرحمن الرحيم

﴿وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ﴾

حزب التحرير
HIZB UT TAHRIR

Toleo Na: 1447 H / 020 | Jumatano, 30 Rabi' II 1447 H | 22/10/2025 M


## Taarifa kwa Vyombo vya Habari

### Mayahudi Hawaheshimu Maagano Wala Hawawezi Kuaminiwa, Na Wapatanishi Si Waaminifu
### (Imetafsiriwa)

Umbile la Kiyahudi limekiuka makubaliano ya kusitisha mapigano dhidi ya Gaza zaidi ya mara 80, na kusababisha mashahidi wengi na majeraha, pamoja na kubomolewa kwa nyumba na uharibifu wa mali. Waziri mkuu wa umbile la Kiyahudi hata alijisifu kwamba aliangusha tani 153 za mabomu kwenye Ukanda wa Gaza kwa siku moja.

Kuhusu wapatanishi, kiongozi wao, Trump, anawakilisha dola kubwa zaidi ya kikoloni, adui wa Mwenyezi Mungu, Mtume Wake, na Waislamu. Anajigamba kwamba amewapa Mayahudi silaha zenye nguvu zaidi. Kamwe haachi kutoa vitisho vya kuiangamiza Hamas ikiwa haitatimiza makubaliano hayo, akipuuza ukweli kwamba mshirika wake wa karibu, Netanyahu, ndiye anayekiuka makubaliano na kuvunja maagano kila wakati, kwa kisingizio chochote dhaifu, kama umbile lake la kinyama.

Ama kuhusu wapatanishi wengine, tuseme nini? Wao ndio waliokaa kimya kwa miaka miwili mizima wakati wa vita vya Mayahudi dhidi ya Gaza, wakiwa kimya kama wafu. Hawakukata hata mafungamano yao na umbile lao la kihalifu. Kwa kweli, baadhi yao walilipa silaha, vifaa, na mahitaji mengine muhimu ya uhai. Wapatanishi hao wanaojisifu kuhusu kutoa msaada kwa watu wa Gaza si waaminifu. Badala yake, wanaegemea  zaidi upande wa umbile la Kiyahudi na watiifu zaidi kwa bwana wao, Amerika.

Hizb ut Tahrir imesema katika machapisho yake kwamba makubaliano haya "mtego", ikimaanisha kwamba yamejaa mianya ambayo umbile la Kiyahudi linaweza kutumia ili kuhalalisha uvunjaji wake wa makubaliano. Hili limethibitishwa na wachambuzi wengi, pamoja na ukweli kwamba historia ya Mayahudi imejaa giza kwa uvunjaji wa maagano na makubaliano, kuanzia kwa kuwaua manabii wao, kupitia historia yao nyeusi na Mtume wa Mwenyezi Mungu, Muhammad (saw), kisha tabia yao barani Ulaya hadi walipowalazimisha kuishi katika majimbo, na kuwawekea sheria za ubaguzi wa rangi ambazo kwazo waliwatenga, na haswa kwa historia yao chafu nchini Palestina na Lebanon.

**Enyi Waislamu:** Maadui zenu wanajua kwa hakika kwamba hawawezi kukabiliana nanyi katika vita halisi vinavyoongozwa na viongozi wenye ikhlasi. Msiba wenu uko kwa watawala wenu, wanaowatumikia mabwana zao, nchi za kikoloni, na umbile katili la Kiyahudi. Hawajali haki zenu, wala hawahifadhi heshima yenu, na wanakula njama na maadui zenu dhidi yenu. Kwa hivyo, jifunzeni kutokana na kinachoendelea, fanyeni uamuzi, na fanyeni kazi pamoja na Hizb ut Tahrir ili kusimamisha Khilafah Rashida ya pili kwa njia ya Utume, kwani ndani yake imo izza yenu na kupitia kwake umo ushindi dhidi ya maadui zenu. Mwenyezi Mungu (swt) asema:

[قَاتِلُوهُمْ يُعَذِّبْهُمُ اللّهُ بِأَيْدِيكُمْ وَيُخْزِهِمْ وَيَنصُرْكُمْ عَلَيْهِمْ وَيَشْفِ صُدُورَ قَوْمٍ مُّؤْمِنِينَ،وَيُذْهِبْ غَيْظَ قُلُوبِهِمْ وَيَتُوبُ اللّهُ عَلَى مَن يَشَاءُ وَاللّهُ عَلِيمٌ حَكِيمٌ]

**"Piganeni nao, Mwenyezi Mungu awaadhibu kwa mikono yenu, na awahizi na akunusuruni muwashinde, na avipoze vifua vya kaumu ya Waumini, * Na aondoe hasira ya nyoyo zao. Na Mwenyezi Mungu humkubalia toba ya amtakaye. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujua Mwenye hikima."** [At-Tawbah: 14-15]

**Afisi Kuu ya Habari**
**ya Hizb ut Tahrir**

المكتب الإعلامي المركزي حزب التحرير HIZB-UT-TAHRIR Central Media Office


**Tovuti:** www.hizb.net
**Pepe:** info@hizb.net

**Tovuti Rasmi ya Hizb ut Tahrir:**
www.hizb-ut-tahrir.org
**Tovuti ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir:**
www.hizb-ut-tahrir.info